SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI, NISHATI NA MADINI
MHESHIMIWA

SULEIMAN MASOUD MAKAME

KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
KWA MWAKA WA FEDHA

2021/2022

**MEI, 2021**

## YALIYOMO


YALIYOMO .................... ii
ORODHA YA VIAMBATISHO .................... iii
VIFUPISHO VYA MANENO .................... iv
1.0 UTANGULIZI .................... 1
2.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2020/2021 .................... 7
2.1 UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU .................... 8
2.2 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2020/2021 .................... 10
3.0 MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 .................... 24
4.0 MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 .................... 35
5.0 HITIMISHO .................... 36

# ORODHA YA VIAMBATISHO


Kiambatisho nambari 1: Upatikanaji wa Fedha na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ............... 40

Kiambatisho nambari 2: Makusanyo ya WMNM kwa mwaka wa fedha 2020/2021 .................................... 42

Kiambatisho nambari 3: Pampu na Mota zilizofanyiwa matengenzo kwa Unguja na Pemba .... 43

Kiambatisho nambari 4: Mota na Pampu mpya zilizonunuliwa na kufungwa .................................. 44

Kiambatisho nambari 5: Shehia zilizonufaika na Huduma ya Maji safi na Salama kwa Unguja na Pemba ........................................................................................... 45

Kiambatisho nambari 6: Maeneo yaliyofanyiwa Utanuzi na Ukarabati wa Mtandao wa maji ................. 46

Kiambatisho nambari 7: Orodha ya wawekezaji walioonesha nia ya kuekeza katika miradi mbali mbali Zanzibar ........................................................... 47

Kiambatisho nambari 8: Maeneo yaliyofanyiwa masawazisho ya umeme mdogo ....... 48

Kiambatisho nambari 9: Maeneo mapya yaliyofikishiwa huduma ya umeme Zanzibar .............. 50

Kiambatisho nambari 10: Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ............... 51

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| WMNM | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| SDGs | Sustainable Development Goals (Malengo ya Maendeleo Endelevu) |
| MKUZA | Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| TZS | Tanzania Shillings (Shilingi ya Tanzania) |
| ZURA | Zanzibar Utility Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za |
| Maji na | Nishati Zanzibar) |
| ZAWA | Zanzibar Water Authority (Mamlaka ya Maji Zanzibar) |
| ZECO | Zanzibar Electricity Corporation (Shirika la Umeme la Zanzibar) |
| ZUWSP | Zanzibar Urban Water Service Project |
| ZEST | Zanzibar Energy Sector Transformation (Mabadiliko ya Sekta ya Nishati Zanzibar) |
| JUWAMAZA | Jumuiya ya Wamiliki wa Mashamba Zanzibar |
| SMT | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| LPG | Liquified Petroleum Gas |

# 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu, likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili, kuzingatia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) mwingi wa rehema kwa kuweza kutukutanisha katika kikao hiki adhimu cha kujadili Bajeti tukiwa wenye afya njema. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuzilinda afya zetu sisi na familia zetu. Vile vile, namuomba atupe uwezo na nguvu za kuijadili, kuichangia na hatimae kuipitisha Bajeti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee nampongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa anayofanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar. Kwa hakika, ndani ya kipindi kifupi tokea kuingia madarakani sisi wote tumekuwa mashuhuda wa kasi ya Awamu ya Nane katika kuwatumikia wananchi

na kupiga vita rushwa pamoja na kusimamia uwajibikaji na ukusanyaji wa mapato katika nchi yetu.

4. **Mheshimiwa Spika,** Rais wetu amekuwa Kiongozi wa mfano kwa kuwa karibu zaidi na wananchi, watendaji na wafanyabiashara mbali mbali. Hali hii imepelekea kuongezeka kwa uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Serikali. Aidha, ameimarisha azma ya Serikali ya kushirikiana na wafanyabiashara na taasisi binafsi katika kuimarisha maendeleo na kufikia Uchumi wa Buluu. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie hekima na busara na amjaalie afya njema yeye na familia yake, ili azidi kuleta maendeleo kwa taifa letu.

5. **Mheshimiwa Spika,** nachukua nafasi hii kumpongeza na kumtakia afya njema Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdallah, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa namna ambavyo wanamsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku ya kuongoza na kusimamia shughuli za Serikali katika kipindi hiki.

6. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa nimpongeze mama yangu, kiongozi wangu shupavu na mwenye hekima na busara, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuapishwa kushika madaraka ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni imani yangu kuwa ataendeleza mambo yote mazuri waliyoyaasisi yeye na Rais wa Awamu ya Tano Marehemu John Pombe Magufuli. Namuombea kwa Mwenyezi Mungu amzidishie afya njema yeye na familia yake, ili aendelee kuwatumikia wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuimarisha umoja na mshikamano wa Nchi yetu.

7. **Mheshimiwa Spika,** nakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Baraza la Kumi la Wawakilishi. Ni Imani yangu kuwa, kwa kutumia uzoefu ulionao wa kuongoza Muhimili huu utaendelea kufanya kazi kwa weledi mkubwa na kuendesha mijadala kwa ufanisi. Kadhalika, nampongeza Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza hili kwa kuchaguliwa kushika nyadhifa hizo. Ni Imani yangu kuwa watakusaidia ipasavyo katika kuendesha chombo hiki muhimu kwa maendeleo ya wananchi.

8. **Mheshimiwa Spika,** naomba kumpongeza Mheshimiwa Mohamed Ahmada Salum, Mwakilishi wa Jimbo la Malindi kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Khuzaima Mbarak Tahir Mwakilishi wa Viti Maalum Vijana Mkoa wa Mjini kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa kuteuliwa kuunda Kamati hiyo. Tokea tumeanza kufanya kazi na Kamati hiyo tumeshuhudia ushirikiano mkubwa miongoni mwetu ambao umepelekea kuimarika kwa utendaji wetu. Ni imani yangu kuwa tutaendelea kushirikiana katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa.

9. **Mheshimiwa Spika,** natoa pongezi kwa Mheshimiwa Miraji Khamis Mussa (Kwaza) kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Kadhalika, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa kuteuliwa kuunda Kamati. Tunawashukuru kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri wanaotupatia katika kutekeleza majukumu yetu. Tunawaahidi kuwa tutaendelea kuwapatia ushirikiano mkubwa ambao utafanikisha kutekeleza majukumu yetu.

10. **Mheshimiwa Spika,** kwa unyenyekevu mkubwa natoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniamini na kunipa jukumu la kuwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar. Hii ni heshima kubwa kwangu binafsi na wananchi wote wa Jimbo la Chonga. Namuahidi kuwa nitafanya kazi kwa nguvu na uwezo wangu wote, ili kuhakikisha kuwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini inatoa huduma stahiki kwa wananchi wa Zanzibar.

11. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa nawapongeza wananchi wa Jimbo letu la Chonga kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mwakilishi wao. Nawaahidi kuwa nitafanya kazi nao bega kwa bega katika kuleta maendeleo na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazokabili Jimbo letu.

12. **Mheshimiwa Spika,** naomba kumalizia salamu zangu za pongezi kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Baraza la Kumi la Wawakilishi. Tumeingia katika Chombo hiki adhimu kwa lengo la kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar katika maeneo yetu. Safari hii itakamilika baada ya miaka mitano kupita ambapo wananchi watatufanyia tathmini ya utendaji wetu na kutufanyia maamuzi.

Napenda kuwakumbusha Ibara ya 255 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, naomba kunukuu. "Ni ukweli usionashaka kuwa, ili CCM iendele kukubalika na kuaminiwa na wananchi na kupewa ridhaa ya kuongoza nchi yetu, upo umuhimu mkubwa wa Viongozi wa CCM, kuwa karibu na wananchi kwa kuwatembelea, kusikiliza kero zao na kushirikiana nao katika kuzipatia majawabu" . Kwa kuwa sisi ni miongoni mwa Viongozi wa CCM, natoa wito kwetu sote kuwatembelea wananchi na kufanya kazi nao kwa karibu na kutekeleza ahadi zote tulizowaahidi.

13. **Mheshimiwa Spika,** Nichukue fursa hii, kutoa salamu za pole na kuwaombea viongozi wetu wakuu, waliotangulia mbele ya haki kipindi kifupi kilichopita. Kwa hakika vifo vya viongozi hao wapendwa hayati John Pombe Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Marehemu Maalim Seif Sharif Hamadi aliyekuwa Makamu wa kwanza wa Rais wa Zanzibar vimeleta simanzi na majozi makubwa kwa familia, watanzania, waafrika na ulimwengu mzima.

14. Tutawakumbuka daima kwa namna walivyojitolea kuleta maendeleo kwa watanzania na ujasiri wao pamoja na kushajihisha kuchapa kazi.

15. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba uniruhusu niwasilishe Utekelezaji wa Programu za Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2020/2021.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2020/2021

16. **Mheshimiwa Spika,** Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini zimetekeleza Bajeti ya Mwaka wa fedha 2020/2021 iliyoidhinishwa katika Baraza lako Tukufu kwa iliyokuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati. Hivyo, baadhi ya Idara na Taasisi zimerithi bajeti kutoka kwa Wizara hiyo ya zamani kabla ya kuundwa Wizara mpya.

    Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa fedha 2020/2021 imetekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu tatu (3) na Programu Ndogo sita (6) chini ya Fungu N03. Programu Kuu hizo ni:-

    i. Programu Kuu: Usimamizi wa Huduma za Maji,
    ii. Programu Kuu: Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini na
    iii. Programu Kuu: Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM.

17. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Programu hizi, umezingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020-2050, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Mwaka 2020 – 2025, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA III), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030, Ahadi alizozitoa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kipindi cha Kampeni za Uchaguzi, Hotuba ya Mheshimiwa Rais katika ufunguzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi na Maagizo ya Utendaji kwa Mawaziri na Makatibu Wakuu aliyoyatoa wakati wa kuwaapisha.

## 2.1 UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU

18. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilijipangia kutumia jumla ya TZS bilioni themanini na tisa milioni kumi na saba laki mbili themanini na tisa mia nne ishirini na tano (TZS. 89,017,289,425). Kati ya hizo TZS bilioni tano milioni mia tano ishirini na sita laki saba hamsini na tatu mia nne ishirini na tano (TZS. 5,526,753,425) kwa ajili ya kazi za kawaida na TZS bilioni themanini na tatu milioni mia nne tisini laki tano thelathini na sita elfu (TZS. 83,490,536,000) kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

19. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2021 Wizara imeingiziwa jumla ya TZS bilioni thelathini na saba milioni mia nne themanini na nne laki tisa sitini na tisa mia tano sabini na mbili (TZS. 37,484,969,572) sawa na wastani wa asilimia 42 ya fedha zote. Kati ya hizo, TZS bilioni tatu milioni mia mbili kumi na sita laki saba sabini na mbili mia moja ishirini na saba (TSZ. 3,216,772,127) kwa kazi za matumizi ya kawaida na bilioni thelathini na nne milioni mia mbili sitini na nane laki moja tisini na saba mia nne arubaini na tano (TZS. 34,268,197,445) kwa kazi za miradi ya maendeleo (Kiambatisho Namba 1 kinatoa ufafanuzi).

20. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilijipangia kukusanya kupitia taasisi zake jumla ya TZS bilioni mia moja themanini na nne milioni mia saba themanini na tisa laki mbili arubaini na tano mia tisa kumi na nne (TZS. 184,789,245,914). Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 Wizara imekusanya jumla ya TZS bilioni mia moja na tisa milioni mia tisa hamsini na sita laki mbili tisini mia tisa themanini na tisa (TZS. 109,956,290,989) sawa na wastani wa asilimia 60 ya makadirio. Mchanganuo halisi wa fedha zilizokusanywa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 unaonekana katika Kiambatisho Namba 2.

## 2.2 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2020/2021

21. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Machi, 2020/2021, Wizara ya Maji, Nishati na Madini ilitekeleza Programu zake kwa ufanisi na kupata mafanikio yafuatayo:-

22. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imefanikiwa kurejesha huduma za maji safi na salama kwa wananchi waliokosa huduma hiyo katika baadhi ya maeneo ya Unguja na Pemba. Aidha, Wizara imefanikiwa kurejesha huduma ya maji safi na salama katika baadhi ya maeneo yaliyokuwa na upungufu wa huduma ya maji. Hii ni kutokana na kufanya matengenezo ya pampu na mota katika vituo 39 vilivyokuwa na hitilafu. Kati ya hivyo, vituo 17 kwa upande wa Unguja na 22 kwa upande wa Pemba. Kiambatisho Namba 3 kinatoa ufafanuzi.

    Vile vile, pampu na mota mpya 19 zimenunuliwa na kufungwa katika visima ambavyo pampu na mota zake ziliungua. Kiambatisho Namba 4 kinatoa ufafanuzi. Kutokana na ununuzi, ufungwaji na matengenezo ya mota na pampu, Jumla ya Shehia 58 zimenufaika na huduma ya maji

safi na salama kama zinavyoonekana katika Kiambatisho Namba 5.

23. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeimarisha usimamizi wa visima kwa kuvifanyia usafi mara kwa mara visima vinavyotoa huduma kwa wananchi. Hatua hii inalenga kuhakikisha kuwa visima vinafanya kazi katika kiwango halisi cha utoaji wa huduma na ubora wa maji. Jumla ya visima 31 kwa Unguja na 21 kwa Pemba vimefanyiwa usafi kati ya visima 85 vilivyohitajika kusafishwa. WMNM inafanya kazi kwa bidii kuhakisha kuwa huduma ya maji safi na salama inapatikana kwa wananchi kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 186 (a) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025.

24. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Wizara imefanikiwa kupunguza upotevu wa maji katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba kwa kuziba mivujo. Jumla ya mivujo 1,489 imezibwa katika maeneo ya Wilaya ya Kaskazini A na B, Magharibi A na B, Mjini, Kati na Kusini Unguja pamoja na mivujo 1,382 katika Wilaya ya Wete, Micheweni, Chake Chake na Mkoani kwa upande wa Pemba.

25. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imefanikiwa kuongeza Mtandao wa maji Zanzibar kwa kuufanyia

Upanuzi na Ukarabati wa masafa ya kilomita 13.96 kwa Unguja na kilomita 14.75 kwa Pemba (Kiambatisho namba 6 kwa ufafanuzi).

26. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Wizara imefanikiwa kuongeza idadi ya watumiaji wa huduma ya maji safi na salama majumbani. Ongezeko hilo limetokana na usajili wa wateja wapya pamoja na ufungaji wa mita. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2020/2021 jumla ya wateja wapya 3,090 wamesajiliwa (Unguja 2,801 na Pemba 289). Aidha, Wizara imefanikiwa kufunga mita 1,135 katika maeneo ya Wilaya ya Kaskazini "A", Kaskazini "B", Magharibi "A", Magharibi "B," Mjini, Kati na Kusini kwa Unguja.

27. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini itaendelea na jitihada za kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kupitia kulipia huduma ya maji, ili kuiwezesha sekta ya maji kujiendesha kwa ufanisi. Jambo hili limewekewa msisistizo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Ibara ya 186(b) isemayo "Kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na kuimarisha usalama wa fedha kwa kufunga mita kwa watumiaji wa maji pamoja na kutumia huduma za kielektroniki katika kulipia huduma hizo". Natoa wito kwenu Waheshimiwa kuendelea kushirikiana na Wizara hii, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

28. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Wizara katika kipindi cha Julai - Machi, 2020/2021, imefanikiwa kuhamasisha jamii katika maeneo 81 juu ya umuhimu wa kulipia huduma ya maji safi na salama pamoja na utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji. Uhamasishaji huo umefanyika kupitia vipindi 15 vya TV na Radio, Mitandao ya kijamii na Mikutano. Kati ya maeneo 81 yaliyopatiwa uelewa huo ni 61 kwa Unguja na 20 kwa Pemba. Matokeo ya uhamasishaji huo ni kwamba wananchi wa maeneo ya mjini wamekuwa na muamko mkubwa wa kulipia huduma ya maji. Jitihada hizo zinafanyika kwa lengo la kuhakisha jamii inatambua umuhimu wa kulipia huduma ya maji na uhifadhi wa vyanzo vya maji kama ilivyoelezewa katika Ibara ya 186 (c) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025.

    Vile vile, kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2020/2021, Wizara ya Maji, nishati na Madini imefanikiwa kupunguza uharibifu wa vyanzo vya maji kwa kuyawekea uzio maeneo tisa (9) ya Unguja.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kuhakikisha kuwa Zanzibar inakuwa na nishati ya uhakika pamoja na kutekeleza Ibara ya 175 (a) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025, Wizara ya Maji, Nishati na Madini

imefanya mazungumzo na wawekezaji wa Nishati Mbadala na Makampuni mbali mbali yakiwemo; ZBS INVESTMENT, ESR, TANLUX Co. Investmet, IIAN TECH, TBEA, IDEAL GAS, KUNSONS CONSULTING, MPS, UNIHA, PERNTELS Co. Limited na ICON PBV. Wawekezaji hao wameonesha nia ya kuwekeza Zanzibar katika maeneo tofauti ya nishati ikiwemo nishati mbadala ya umeme wa jua, umeme wa takataka na umeme wa upepo. Ufafanuzi kuhusu maeneo ambayo Wawekezaji hao wameonesha nia ya kuwekeza unapatikana katika Kiambatisho Namba 7

30. **Mheshimiwa Spika,** WMNM inaendelea kuandaa mfumo wa kukusanya takwimu za nishati baada ya kukamilika kwa Mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za Nishati "Energy Statistic DataBase" . Taarifa hizo zinakusanywa kila baada ya miezi mitatu kutoka ZURA, ZECO na Idara ya Misitu na kuziingiza katika mfumo huu wa Utunzaji wa Takwimu. Takwimu hizo zinasaidia kupata taarifa za uhakika ambazo zinatumika katika mipango mbali mbali ya maendeleo katika sekta ya Nishati.

31. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) imehakikisha kwamba

wanatoa huduma bora kwa wananchi. Hatua hiyo imefikiwa kutokana na kuimarisha udhibiti wa huduma zinazotolewa kwa mujibu wa sheria. Ukaguzi wa mara kwa mara wa vituo vya mafuta umekua ukifanyika ambapo vituo vyote 81 vya mafuta vimekaguliwa. Hali hiyo, imepelekea kupungua kwa kiasi kikubwa tatizo la uchakachuaji wa mafuta kati ya bidhaa moja ya mafuta na nyengine. Vile vile, imepunguza malalamiko ya kuharibika kwa vyombo vya usafiri kutokana na mafuta yaliyochakachuliwa.

32. **Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi huo, pia ilibainika kuwa baadhi ya vituo vinakiuka Kanuni ya Usimamizi ya Vituo vya Mafuta ya mwaka 2019. Hali hiyo imepelekea Wizara kuvifungia Vituo viwili vya Unguja kufanya kazi kutokana na kukiuka matakwa ya Kanuni hiyo. Wamiliki wa vituo hivyo wametakiwa kurekebisha kasoro zilizobainika, ili warejeshewe leseni za uendeshaji wa biashara hiyo. Ukiukwaji mkubwa umejikita katika masuala ya miundombinu, usalama pamoja na afya ya wafanyakazi na wananchi kwa ujumla.

33. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Wizara imefanikiwa kutoa elimu kwa jamii juu ya kuanzishwa kwa ZURA na majukumu inayotekeleza, matumizi sahihi ya nishati

ikiwemo gesi na umeme na bei halisi za bidhaa za mafuta na gesi. Elimu hiyo hutolewa kupitia vyombo vya habari, mikutano ya wadau na machapisho. Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 20220/2021, jumla ya vipindi kumi (10) vya Televisheni (TV) na vipindi kumi (10) vya Radio vimerushwa hewani. Vile vile, Mikutano tisa (9) na Waandishi wa Habari, mkutano na Waheshimiwa Wawakilishi mmoja pamoja na kutoa machapisho 10,782.

34. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Wizara kupitia ZURA imefanikiwa kusimamia vyanzo vyake vya mapato kwa kiasi kikubwa na kupelekea kuongezeka kwa kasi ya ukusanyaji wa mapato. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2020/2021, ZURA imefanikiwa kukusanya Jumla ya TZS bilioni kumi na mbili milioni mia sita arubaini na saba na laki tisa (TZS. milioni 12,647.9) sawa na asilimia 103 ya mapato iliyojipangia kukusanya kwa kipindi hicho. Vile vile, ZURA inaendelea kutoa gawio Serikalini la TZS milioni mia tano (500,000,000) kila mwezi.

35. **Mheshimiwa Spika,** ZURA imeandaa utaratibu wa kupokea, kuchunguza na kuamua malalamiko ya wateja kuhusiana na huduma zinazotolewa kwa mujibu wa Sheria yake. Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2020/2021, jumla ya malalamiko 34

yamepokelewa. Malalamiko hayo yalihusisha utoaji wa huduma za mafuta, umeme na usambazaji wa huduma za maji. Malalamiko 31 yamefanyiwa kazi na ufumbuzi wake umepatikana, na matatu yanaendelea kufanyiwa kazi.

36. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) imefanikiwa kuongeza watumiaji wa huduma ya umeme hapa Zanzibar. Hii imetokana na kupunguza bei ya kuunganisha umeme kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 50.

    Punguzo hilo ni kutoka TZS. 464,000 kufikia TZS. 200,000 kwa gharama za uungaji usiozidi mita 30, kutoka TZS. 1,700,000 kufikia TZS. 690,000 kwa gharama za uungaji wa nguzo 1 na kutoka TZS. 2,600,000 kufikia TZS. 1,040,000 kwa gharama za uungaji wa nguzo 2. Hatua hii imefanywa ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 175 (g) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025.

37. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya umeme. Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2020/2021, jumla ya nguzo mbovu 2,946 ambazo ni wastani wa asilimia 164 zimebadilishwa kati ya nguzo 1,800 zilizopangwa kubadilishwa. Vile vile, Wizara

imefanya ukaguzi wa transfoma katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba. Jumla ya transfoma 1,131 sawa na asilimia 71 ya transfoma 1,584 zimekaguliwa. Katika ukaguzi huo, transfoma 100 zilibainika kuwa na hitilafu na zimefanyiwa masawazisho (92 Unguja, 8 Pemba).

38. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kupunguza matatizo ya umeme mdogo kwa wananchi ambao waliokuwa wanakabiliwa na tatizo hilo. Jumla ya maeneo 44 kwa upande wa Unguja sawa na wastani wa asilimia 183 ya maeneo 24 yaliyopangwa awali. Kwa upande wa Pemba maeneo 12 sawa na asilimia 100 yameshaondolewa tatizo hilo (Kiambatisho Namba 8 kinatoa ufafanuzi kuhusu maeneo yaliyopatiwa huduma hiyo). Kadhalika, Wizara imekusudia kumaliza tatizo hilo kwa muda mfupi. Katika kufanikisha hilo, Wizara imeandaa Mpango mkakati wa kurekebisha matatizo hayo ndani ya kipindi cha miezi mitatu (Mei hadi Julai, 2021).

39. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2020/2021, Wizara imefanikiwa kupeleka umeme katika maeneo mapya 29 kwa Unguja na 20 kwa Pemba (Kiambatisho Namba 9 kinatoa ufafanuzi). Vile vile, jumla ya wateja wapya 15,605 wameunganishiwa umeme sawa na wastani wa asilimia 81 ya

wateja 19,200 waliopangwa kuunganishiwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Chama cha Mapinduzi kimeahidi kuwa kitaimairisha shughuli za usimamizi wa huduma za umeme na usambazaji wa nishati katika vijiji 305 kwa Unguja na Pemba (Ibara ya 175(b) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025).

40. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini imeandaa utaratibu mpya wa upatikanaji wa mchanga. Utaratibu huo unahusisha kuchimba mchanga katika mashamba ya watu binafsi. Wamiliki wa mashamba hayo, hutakiwa kuwasilisha Wizarani vielezo vinavyoonesha uhalali wa umiliki wao wenyewe au Jumuiya yao (JUWAMAZA). Vielelezo hivyo, hufanyiwa uhakiki na Mamlaka husika, ili kujiridhisha juu ya uhalali wake. Baada ya hatua hiyo, Serikali hufunga mkataba na wamiliki wa mashamba hayo na kazi ya kuchimba mchanga huanza. Kupitia utaratibu huo, mmiliki wa shamba anapata TZS. 3,000 katika TZS. 10,000 ambayo ni bei ya sasa kwa kila tani na Shilingi 7,000 zilizobakia zinarudi Serikalini.

41. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Serikali imeanzisha utaratibu mpya wa kuwapatia mchanga wananchi kwa ajili ya matumizi yao. Utaratibu huo unamtaka mtu ambae anahitaji mchanga kufika Wizarani

akiwa na vitambulisho vyake. Baada ya kukamilisha taratibu zote kwa mujibu wa maelekezo ya Wizara, muhusika hutakiwa kulipia Benki kiasi cha mchanga anachokihitaji kwa gharama nilizozieleza hapo awali. Utaratibu huu unadhamiria kupunguza mrundikano wa mchanga usio na matumizi ikizingatiwa kuwa nchi yetu inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa mchanga.

42. **Mheshimiwa Spika,** suala la udhibiti wa mchanga ni suala la lazima hasa katika nchi za visiwa kama iliyo Zanzibar. Kwa kutambua ukweli huo, Wizara inajipanga kuhakikisha kuwa inaweka utaratibu mzuri wa kutumia rasilimali hiyo, kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadae. Vile vile, kwa kutambua kuwa ni vigumu kurejesha katika hali yake ya kawaida maeneo yaliyochimbwa rasilimali zisizorejesheka, Wizara itaweka utaratibu mzuri wa kufanya matumizi mbadala ya maeneo ya mashimo yaliyochimbwa rasilimali hizo. Utaratibu huo utawezesha maeneo hayo kutumika kwa matumizi yenye kuleta tija ya kiuchumi, kijamii pamoja na kuweka vizuri haiba ya maeneo hayo kama ambavyo imeelekezwa katika Ibara ya 151 (b) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025.

43. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha tunatekeleza maagizo tuliyopewa na

Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ikiwemo kuwajibika kazini, WMNM imefanya vikao vya wafanyakazi wa Idara na Taasisi zote zilizo chini yake. Katika vikao hivyo, wafanyakazi wamesisitizwa kuwajibika ipasavyo katika kutekeleza majukumu yao na kutokufanya kazi kwa mazoea na badala yake wafanye kazi kwa uweledi na kujituma. Hali hiyo itaipelekea Wizara na Serikali kiujumla kufikia malengo iliyojipangia ya kuwahudumia wananchi wa Zanzibar.

44. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kufanya mapitio ya miundo ya Idara na Taasisi zote zilizo chini yake, ili iweze kuendana na mahitaji ya Serikali katika kuwahudumia wananchi. Mapendekezo ya miundo ya ZAWA na ZECO imewasilishwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa hatua zaidi. Aidha, Wizara inaendelea na kazi ya kuandaa Mkataba wa Huduma kwa Umma. Rasimu ya awali ya Mkataba huo tayari imekamilika na imeshajadiliwa katika kikao cha wadau. Hatua inayofuata ni kuwasilishwa katika Kamati ya Uongozi ya WMNM kwa hatua stahiki. Kukamilika kwa Mkataba huu kutaiwezesha Wizara kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi na wananchi watapata fursa ya kutathmini namna huduma zinavyotolewa.

45. **Mheshimiwa Spika,** katika kuyafanyia kazi malalamiko yanayowakabili wananchi pamoja na wafanyakazi wa Wizara, WMNM imeandaa utaratibu maalum unaowawezesha wananchi na wafanyakazi kuonana na Mheshimiwa Waziri na kuwasilisha malalamiko yao. Utaratibu huo umepangiwa muda maalum ambapo siku ya Jumanne na Alhamis ni kwa ajili ya kuwasiliza wananchi na Ijumaa wafanyakazi wa Wizara. Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2020/2021, Wizara imepokea jumla ya malalamiko 34. Kati ya hayo 26 yamepatiwa ufumbuzi na 8 yanaendelea kufanyiwa kazi.

46. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa Sheria na Sera zinazosimamiwa na WMNM zinaendana na mahitaji ya sasa, Wizara inazifanyia marekebisho Sheria mbali mbali za Taasisi zake. Sheria hizo ni Sheria Namba 3 ya Kuanzisha Shirika la Umeme ya mwaka 2006, Sheria Namba 4 ya Kuanzisha Mamlaka ya Maji Zanzibar ya mwaka 2006 na Sheria Namba 7 ya Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar ya mwaka 2013. Matarajio yetu ni kupitishwa katika mwaka wa fedha 2021/2022.

47. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuratibu vikao na mikutano ya kisekta na mashirikiano baina ya Wizara za SMT na

Taasisi nyengine za ndani na nje ya nchi. Kutokana na mashirikiano hayo, WMNM imeweza kupata uzoefu wa namna ya kutatua changamoto za usimamizi na usambazaji wa huduma za maji na nishati Zanzibar. Mnamo tarehe 18 hadi 19 Februari, 2021 Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar ilikutana na Wizara ya Maji ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufanya kikao cha kubadilishana uzoefu wa kiutendaji. Katika kikao hicho pamoja na mambo mengine mada mbali mbali zilijadiliwa ikiwemo Usimamizi wa ubora wa maji, Mipango ya kimkakati ya huduma za maji pamoja na Usimamizi na Uendelezaji wa Raslimali za maji.

48. **Mheshimiwa Spika,** WMNM imeandaa pendekezo la utafiti wa kutathmini kiwango cha maji kilichopo chini ya ardhi hapa Zanzibar. Matokeo ya utafiti huo, yatapelekea kujua kima halisi na uasili wa maji ya Zanzibar, kubainisha aina ya miamba iliyopo Zanzibar. Vile vile, utafiti huo utaiwezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuelekea katika Uchumi wa Buluu ikiwa na uhakika na usalama wa matumizi ya maji yake

49. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, WMNM imeandaa pendekezo la Utafiti wa kutathmini wastani wa matumizi ya maji safi na salama kwa wakaazi wa Zanzibar. Utafiti huo utahusisha

mahitaji halisi ya maji kwa kila kaya, maeneo ya uwekezaji, mahoteli, viwanda, umwagiliaji, mifugo, Taasisi za Serikali, Kijamii na Kiraia. Kwa ujumla tafiti hio inalengo la kufahamu mahitaji halisi ya maji kwa wananchi wa Unguja na Pemba, ili kuhakikisha huduma hiyo inapatikana bila ya usumbufu.

## 3.0 MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

50. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imejipangia kutekeleza bajeti yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:-

    i. Kutambua kiwango halisi cha maji kilichopo chini ya ardhi kwa Unguja na Pemba,
    ii. Kuimarisha miundombinu ya maji iliyopo na kuweka miundombinu mipya,
    iii. Kutambua mahitaji halisi ya maji, nishati na madini kwa Zanzibar,
    iv. Kuimarisha miundombinu ya ukusanyaji wa mapato,
    v. Kutafuta Nishati Mbadala ya umeme kwa mahitaji ya Zanzibar na
    vi. Kuweka utaratibu mzuri wa upatikanaji wa mafuta na gesi Zanzibar.

51. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini itatekeleza vipaumbele hivyo kupitia Programu Kuu tatu (3) na Programu Ndogo sita (6) zifuatazo:-

## A. Programu Kuu PN0301: Usimamizi wa Huduma za Maji

52. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni kusimamia utafutaji na usambazi wa rasilimali maji kwa watumiaji wa maji Zanzibar. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuhakikisha kuwa huduma za za maji safi na salama zinakuwa endelevu na za uhakika kwa maendeleo ya shughuli za kijamii na kiuchumi Zanzibar. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo moja ambayo ni:-

### Programu Ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji.

53. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, WMNM imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-
    i. Kuendeleza na kusimamia matumizi ya Rasilimali za Maji kulingana na Sera ya Maji na mikakati ya kitaifa,
    ii. Kuandaa, kufuatilia, kutathmini na kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na miongozo ya maji Zanzibar,

iii. Kutoa miongozo na elimu kuhusu ulipaji, utunzaji na uhifadhi wa mazingira ya vyanzo vya maji,
iv. Kutoa miongozo kwa wadau kuhusu Usimamizi wa Rasilimali za Maji na
v. Kutafuta ushauri wa kitaalamu kuhusu uvunaji wa maji ya mvua.

54. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii pia itatekelezwa kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ambayo inajukumu la kisheria la kusimamia masuala ya maji hapa Zanzibar.

55. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ZAWA kupitia Programu hii imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-
    i. Kuendeleza kazi za kawaida za matengenezo ya miundombinu ya maji,
    ii. Kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji,
    iii. Kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi bora ya huduma ya maji pamoja na umuhimu wa kulipia huduma za maji,
    iv. Kusajili wateja wapya na kufunga mita za wateja,
    v. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi wa ZAWA,
    vi. Kutoa huduma za uendeshaji wa ofisi na kutoa stahiki za wafanyakazi,

vii. Kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kutumia njia mbali mbali,
viii. Kutekeleza Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar (USD 92.18 Milioni, Exim - India),
ix. Kutekeleza Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira (USD 35 Milioni, Exim – India) na
x. Kuendeleza visima vilivyochimbwa na Mradi wa Ras Al Khaimah.

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka ya Maji Zanzibar imejipangia kukusanya jumla ya TZS bilioni kumi milioni mia nane sabini laki nne tisini na moja na mia mbili (TZS. milioni 10,870,491,200) kutokana na vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni mauzo ya maji na mapato mengineyo.

57. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS bilioni themanini na nne milioni mia sita sabini na saba na laki tatu ishirini na moja elfu (TZS. 84,677,321,000). Kati ya hizo TZS bilioni tatu milioni mia sita na nane na laki mbili (TZS. 3,608,200,000) kwa ajili ya matumizi ya Ruzuku ya Mshahara na TZS bilioni themanini na moja milioni sitini

na tisa na laki moja ishirini na moja elfu (TZS. 81,069,121,000) kwa ajili ya kazi za miradi ya maendeleo zilizopangwa katika Programu hii.

## B. Programu Kuu PNO302: Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini

58. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni kusimamia uzalishaji na usambazi endelevu wa huduma za nishati. Aidha, kusimamia uchimbaji na upatikanaji wa madini kwa wakaazi wa Zanzibar. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuhakikisha kuwa Zanzibar inakuwa na utaratibu mzuri wa upatikanaji wa madini na kuwa na nishati ya uhakika na endelevu kwa maendeleo ya uchumi wa Zanzibar. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili ambazo ni:-

    i. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati.
    ii. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Madini.

59. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii itatekelezwa kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) ambazo zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria. Vile vile, Programu hii itatekelezwa na Idara ya Nishati na Madini.

## A. Idara ya Nishati na Madini

60. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, WMNM kupitia Idara ya Nishati na Madini imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-
    i. Kutoa huduma za kila siku za uendeshaji na utawala katika Idara ya Nishati na Madini,
    ii. Kutoa elimu kwa wananchi wa Zanzibar juu ya maswala ya nishati na madini,
    iii. Kufanya Ufuatiliaji na tathmini wa shughuli zinazotekelezwa na Idara ya Nishati na Madini,
    iv. Kuandaa programu za uelewa kwa wananchi na taasisi juu ya matumizi ya nishati mbadala,
    v. Kukamilisha mapitio ya Sera ya Nishati na utungaji wa Sheria ya Nishati na
    vi. Kuandaa Sera ya Madini.

61. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, Wizara kupitia Idara hii ina jukumu la kusimamia masuala ya nishati pamoja na rasilimali zisizorejesheka ambazo ni mchanga, kokoto, mawe, fusi na vumbi. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kupitia Kitengo cha Usimamizi wa Rasilimali Zisizorejesheka imejipangia kukusanya jumla ya TZS bilioni saba milioni mia saba arubaini na tatu na laki mbili sitini na mbili elfu (TZS. 7,743,262,000). Makusanyo

hayo yanatokana na maombi ya vibali na malipo ya rasilimali hizo.

## B. Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kupitia programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-
    i. Kuendeleza mradi wa Usambazaji wa Umeme mjini na vijijini,
    ii. Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA) – Unguja,
    iii. Kuimarisha Miundombinu ya umeme na kulijengea uwezo Shirika la Umeme Zanzibar,
    iv. Uzalishaji wa umeme kwa kutumia nishati ya jua na kuungia wateja – Pemba (Benki ya Maendeleo ya Afrika - AfDB) na
    v. Kufanya utafiti wa kupata chanzo chengine cha umeme Zanzibar.

63. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Umeme Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2021/2022 limejipangia kukusanya jumla ya TZS bilioni mia moja na sabiini milioni mia saba hamsini na nane laki mbili arubaini na tisa mia saba ishirini na saba (TZS. 170,758,249,727) kutokana na mauzo na huduma zake.

## C. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ZURA kupitia programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-
    i. Kudhibiti huduma za maji na nishati (mafuta, umeme, na gesi ya kupikia – LPG),
    ii. Kuandaa na kukamilisha nyenzo za kusimamia udhibiti katika sekta za Maji na Nishati ikiwemo shughuli za miradi ya uwekezaji wa nishati mbadala ya umeme inayotarajiwa kufanyika Zanzibar,
    iii. Kuajiri washauri elekezi katika kudhibiti Taasisi zinazotoa huduma kwa wananchi, ili kuweza kuzifanikisha Taasisi za ZECO na ZAWA kujiendesha kibiashara kwa kuangalia gharama halisi zinazozalishwa na kukusanywa,
    iv. Kufanya tafiti za kimifumo na miundombinu juu ya uwezo wa ZECO na ZAWA wa kutoa huduma kwa wananchi,
    v. Kuimarisha uendeshaji, mazingira ya kazi kwa wafanyakazi yakiwemo mafunzo na stahiki zao,
    vi. Kushiriki katika mikutano, warsha na makongamano yanayohusu udhibiti wa huduma za maji na nishati kitaifa na kikanda,

vii. Kuanza kutumia mfumo mpya wa taarifa (ZURA UTILITIES INTERGRATED SYSTEM) na maombi ya leseni baina ya Mdhibiti (ZURA) na wadau wake,
viii. Kuendelea kukuza uelewa (Raising Awareness) kwa wananchi kuhusu masuala ya udhibiti wa huduma za maji na nishati Zanzibar,
ix. Kuanza kwa ujenzi wa jengo la Afisi za ZURA kwa upande wa Pemba,
x. Kuandaa vikao vya kawaida na vya dharura vya CRC,
xi. Kuandaa Sera na Sheria la Baraza la Watumiaji,

65. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2021/2022, imejipangia kukusanya jumla ya TZS bilioni kumi na saba na milioni mia mbili (TZS. 17,200,000,000) kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

66. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini iweze kutekelezeka, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS bilioni kumi na mbili milioni mia tatu sitini na tatu laki nne thelathini na saba elfu (TZS. 12,363,437,000) kwa matumizi ya kazi za kawaida na miradi ya maendeleo zilizopangwa katika Programu hii. Kati ya fedha hizo TZS bilioni kumi na

moja milioni mia saba na tatu laki tano kumi na sita elfu (TZS. 11,703,516,000) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na TZS milioni mia sita hamsini na tisa laki tisa ishirini na moja elfu (TZS. 659,921,000) kwa ajili ya kazi za kawaida.

## C. Programu Kuu PNO303: Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM

67. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha uwezo wa kiutendaji na kusimamia stahiki za wafanyakazi wa Wizara. Aidha, Programu hii ina lengo la kuratibu, kuandaa na kutekeleza mipango na miongozo ya Wizara. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika kwa mazingira ya utendajikazi pamoja na mipango inayoakisi mahitaji halisi yaliyopo. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo tatu ambazo ni:-

i. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa WMNM.
ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za WMNM.
iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za WMNM – Pemba.

68. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii, WMNM imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuratibu na kuandaa mikutano ya Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji, Bodi ya Zabuni, Kamati ya Ukaguzi wa Ndani na Wafanyakazi wa WMNM,
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa WMNM kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi,
iii. Kupokea malalamiko ya wananchi na kuyatolea maelezo,
iv. Kulipa mishahara na kuwapatia stahiki nyengine wafanyakazi wa WMNM,
v. Kutoa huduma za uendeshaji wa Wizara,
vi. Kuandaa, Kusimamia na Kufanya Mapitio ya Sera, Sheria na Mipango ya kisekta kwa mujibu wa Vipaumbele vya WMNM,
vii. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini wa shughuli za WMNM,
viii. Kukusanya takwimu za utekelezaji wa Shughuli za WMNM,
ix. Kuratibu na Kukuza mashirikiano ya Kisekta na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za WMNM,
x. Kufanya utafiti wa kubaini kiwango cha maji kilichopo chini ya ardhi ya Unguja na Pemba,
xi. Kufanya utafiti ya kubaini matumizi rasmi ya maji kwa Zanzibar,
xii. Kuandaa Mpango Mkakati wa WMNM na
xiii. Kuandaa na kusimamia Mpangokazi wa Wizara.

69. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya Wizara iweze kutekelezeka, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS bilioni moja milioni mia tano tisini na nne laki nne sabini na tisa elfu (TZS. 1,594,479,000) kwa matumizi ya kazi za kawaida.

## 4.0 MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

70. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Wizara ya Maji, Nishati na Madini kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu za WMNM kwa Fungu N03 yenye jumla ya TZS bilioni tisini na nane milioni mia sita thelathini na tano laki mbili thelathini na saba elfu (TZS. 98,635,237,000). Kati ya fedha hizo TZS bilioni tano milioni mia nane sitini na mbili na laki sita (TZS. 5,862,600,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TZS bilioni tisini na mbili milioni mia saba sabini na mbili laki sita thelathini na saba elfu (TZS. 92,772,637,000) kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

71. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, naomba idhini ya kukusanya TZS bilioni saba milioni mia saba arubaini na tatu laki mbili sitini na mbili elfu (TZS. 7,743,262,000) kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato vinavyosimamiwa na Wizara hii. Mgawanyo wa fedha zitakazotumika kwa utekelezaji wa kila Programu umeainishwa katika Kiambatisho Namba 10.

## 5.0 HITIMISHO

72. **Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine tena napenda kumpongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa namna anavyotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025 kwa vitendo. Sote ni mashahidi kuwa mambo mengi aliyoahidi kuyatekeleza anaendelea kuyatekeleza kwa kasi kubwa. Natoa wito kwetu sisi Wawakilishi wa wananchi tutekeleze ahadi tulizoahidi katika Majimbo yetu, ili tuungane na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa katika kuwatumikia wananchi waliotuchagua na kuitekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 katika muelekeo wa kuifikisha nchi yetu kwenye Uchumi wa Buluu.

73. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati wale wote tunaofanya kazi hizi kwa pamoja akiwemo Katibu Mkuu wa WMNM Dkt. Mngereza Mzee Miraji, Mkurugenzi Mkuu wa ZURA, Mkurugenzi Mkuu ZAWA, Meneja Mkuu ZECO, Wakurugenzi wa Idara na Taasisi za WMNM pamoja na watendaji wote wa WMNM ambao kwa pamoja wamenipa ushirikiano wa hali ya juu katika kuongoza na kutekeleza majukumu ya Wizara na kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanafaidika na huduma zinazotolewa na Wizara hii.

74. **Mheshimiwa Spika,** nawashkuru kwa dhati kabisa washirika wa maendeleo tunaoendelea kufanya nao kazi. Kutokana na ushirikiano huo, Nchi yetu imeweza kutekeleza miradi mbali mbali ya maendeleo ambayo imepelekea Nchi yetu kupiga hatua kubwa katika kutoa huduma kwa wananchi. Washirika hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya EXIM ya India, Serikali ya Norway, Benki ya CRDB Tanzania, Serikali ya Japan, Serikali ya Sweden, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), UNICEF, Serikali ya Marekani na Serikali ya China. Ni matumaini yangu kuwa washirika hawa tutaendelea kufanyanao kazi kwa manufaa ya pande zote mbili.

75. **Mheshimiwa Spika,** kwa nafasi ya kipekee kabisa napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo letu la Chonga kwa kuendelea kunipa ushirkiano na kuunga mkono juhudu za Serikali za kuleta maendeleo. Nawaahidi kuwa ahadi zote nilizowaahidi nitazitekeleza hatua kwa hatua.

76. **Mheshimiwa Spika,** shukrani makhsus nazipeleka kwa wake zangu, wazee wangu na watoto wangu vipenzi, nawashukuru kwa upendo wao, michango yao, uvumulivu wao na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu haya makubwa ya kitaifa. Nakiri kuwa bila ya uvumilivu wao na ushirikiano nisingeweza kutekeleza majuku yangu kikamilifu.

77. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa kuwasilisha Hotuba hii. Kwa heshima kubwa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee, waipitie, waijadili na hatimae waipitishe bajeti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**78. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Mheshimiwa Suleiman Masoud Makame<br>
Waziri wa Maji, Nishati na Madini<br>
Zanzibar.

**Kiambatisho nambari 1: Upatikanaji wa Fedha na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

| PROGRAMU NDOGO | TAASISI | | BAJETI 2020/2021 (000) | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI, 2021 (000) | | | % YA FEDHA ILIYOPATIKA NA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | SMZ | WAHISANI | JUMLA | SMZ | WAHISANI | JUMLA | |
| Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji | Mamlaka ya Maji (ZAWA) | Ruzuku ya Mshahara | 3,626,500 | - | 3,626,500 | 2,719,875 | - | 2,719,875 | 75 |
| | | Fedha za Matumizi Mengineyo | - | - | - | | - | - | - |
| | **Jumla** | | **3,626,500** | **-** | **3,626,500** | **2,719,875** | **-** | **2,719,875** | **75** |
| Usimamizi na Uimarishaji wa huduma za Nishati | Idara ya Nishati na Madini | Fedha za Matumizi Mengineyo | 140,486 | - | 140,486 | 20,581 | - | 20,581 | 15 |
| | | Fedha za Mshahara | 479,072 | - | 479,072 | 289,255 | - | 289,255 | 60 |
| | **Jumla** | | **619,558** | **-** | **619,558** | **309,836** | **-** | **309,836** | **50** |
| Utawala na Uendeshaji wa WMNM | Utumishi na Uendeshaji | Fedha za Matumizi Mengineyo | 432,850 | - | 432,850 | 36,268 | - | 36,268 | 8 |
| | | Fedha za Mshahara | 188,680 | - | 188,680 | 62,530 | - | 62,530 | 33 |
| | **Jumla** | | **621,530** | **-** | **621,530** | **98,798** | **-** | **98,798** | **16** |
| Uratibu za Mipango, Sera na Utafiti | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | Fedha za Matumizi Mengineyo | 217,034 | - | 217,034 | 8,452 | - | 8,452 | 4 |
| | | Fedha za Mshahara | 53,626 | - | 53,626 | 17,376 | - | 17,376 | 32 |
| | **Jumla** | | **270,660** | **-** | 270,660 | **25,828** | **-** | 25,828 | 10 |
| Uratibu wa Utekelezaji wa Shughuli za | Afisi Kuu Pemba | Fedha za Matumizi Mengineyo | 201,204 | - | 201,204 | - | - | - | - |

| PROGRAMU NDOGO | TAASISI | | BAJETI 2020/2021 (000) | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI, 2021 (000) | | | % YA FEDHA ILIYOPATIKA NA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | SMZ | WAHISANI | JUMLA | SMZ | WAHISANI | JUMLA | |
| WMNM-Pemba | | Fedha za Mshahara | 187,303 | - | 187,303 | 62,434 | - | 62,434 | 33 |
| **Jumla** | | | **388,507** | **-** | **388,507** | **62,434** | **-** | **62,434** | **16** |
| **Jumla Kuu** | | | **5,526,755** | **-** | **5,526,755** | **3,216,771** | **-** | **3,216,771** | **58** |
| **Miradi ya Maendeleo** | | | | | | | | | |
| **PROGRAM NDOGO** | **TAASISI** | | **BAJETI 2020/2021 (000)** | | | **FEDHA ZILIZOPATIKANA HADDI MACHI, 2021 (000)** | | | **% YA FEDHA ILIYOPATIKA NA KWA MWAKA** |
| | | | **SMZ** | **WAHISANI** | **JUMLA** | **SMZ** | **WAHISANI** | **JUMLA** | |
| Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji | Mamlaka ya Maji (ZAWA) | Ruzuku ya Mshahara | - | - | - | - | - | - | |
| | | Fedha za Mradi wa Maendeleo | 4,466,220 | 67,129,316 | 71,595,536 | 525,393 | 21,912,804 | 22,438,197 | 31 |
| Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati | Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) | Fedha za Mradi wa Maendeleo | 65,000 | 11,830,000 | 11,895,000 | - | 11,830,000 | 11,830,000 | 99 |
| **Jumla** | | | **4,531,220** | **78,959,316** | **83,490,536** | **525,393** | **33,742,804** | **34,268,197** | **31** |
| **JUMLA YA FEDHA KWA WMNM** | | | | | **89,017,291** | | | **37,484,968** | **42** |

## Kiambatisho nambari 2: Makusanyo ya WMNM kwa mwaka wa fedha 2020/2021

| NA. | TAASISI/ IDARA | MAKADIRIO YA MAPATO (JULAI - JUNI,2020/2021) | MAPATO HALISI (JULAI - MACHI, 2020/2021) | % YA MAPATO HALISI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | IDARA YA NISHATI NA MADINI | 0 | 1,856,154,962 | |
| 2 | ZAWA | 10,452,500,914 | 2,143,900,000 | 21 |
| 3 | ZURA | 16,055,745,000 | 12,647,636,027 | 79 |
| 4 | ZECO | 158,281,000,000 | 93,308,600,000 | 59 |
| **JUMLA** | | **184,789,245,914** | **109,956,290,989** | **60** |

**Kiambatisho nambari 3: Pampu na Mota zilizofanyiwa matengenzo kwa Unguja na Pemba**

| Nam | UNGUJA | PEMBA |
|---|---|---|
| 1. | Bumbwini Makoba | Mchua |
| 2. | Donge Kipange | Chake – 5 |
| 3. | Chukwani hali ya Hewa | Sharifu Ali – 2 |
| 4. | Dimani Pangoni | Matuleni – 1 |
| 5. | Donge Tumbatu | Uwondwe |
| 6. | Kijito Upele-Uzi | Kwa Changawe |
| 7. | Bambi Uroa | Shidi |
| 8. | Donge Tumbatu 1 | Mahuduthi |
| 9. | Mombasa Ofisini | Mlindo |
| 10. | Jambiani Mfumbwi | Wete – 4 |
| 11. | Migombani Jeshini | Tosa – 1 |
| 12. | Bumbwini Uwandani | Daya |
| 13. | Kianga No. U32 | Kilindi |
| 14. | Mwera Msikiti Mzuri N10 | Bimtumwa – 1 |
| 15. | Dimani Pangoni | Ndagoni |
| 16. | Bumbwisudi NB5 | Ziwani |
| 17. | Bumbwisudi NB8 | Gombani – 4 |
| 18. | | Mwambe |
| 19. | | Mkanyageni |
| 20. | | Mjimbini |
| 21. | | Kironjo D |
| 22. | | Kiuyu manda |

**Kiambatisho nambari 4: Mota na Pampu mpya zilizonunuliwa na kufungwa**

| **Nam** | **UNGUJA** |
|---|---|
| 1. | Kiashange Mzungu |
| 2. | Bambi Pongwe |
| 3. | Kipandoni |
| 4. | Migombani Jeshini |
| 5. | Dole Mzungu Punda |
| 6. | Tazari |
| 7. | Kijito Upele |
| 8. | Mjonga kisima kipya |
| 9. | Chumbuni |
| 10. | Masingini |
| 11. | Kajengwa |
| 12. | Kiembesamaki kwa Bakathir |
| 13. | Bumbwini Kidanzini |
| 14. | Mfenesini |
| 15. | Bumbwisudi NB5 |
| 16. | Bumbwisudi NB7 |
| 17. | Bumbwisudi NB8 |
| 18. | Bumbwini Uwandani |
| 19. | Kiashange JP5 – 2 |

**Kiambatisho nambari 5: Shehia zilizonufaika na Huduma ya Maji safi na Salama kwa Unguja na Pemba**

| Nam | UNGUJA | PEMBA |
|---|---|---|
| 1. | Bumbwini Makoba | Mchua |
| 2. | Donge Kipange | Chake – 5 |
| 3. | Chukwani hali ya Hewa | Sharifu Ali – 2 |
| 4. | Dimani Pangoni | Matuleni – 1 |
| 5. | Donge Tumbatu | Uwondwe |
| 6. | Kijito Upele-Uzi | Kwa Changawe |
| 7. | Bambi Uroa | Shidi |
| 8. | Donge Tumbatu 1 | Mahuduthi |
| 9. | Mombasa Ofisini | Mlindo |
| 10. | Jambiani Mfumbwi | Wete – 4 |
| 11. | Migombani Jeshini | Tosa – 1 |
| 12. | Bumbwini Uwandani | Daya |
| 13. | Kianga No. U32 | Kilindi |
| 14. | Mwera Msikiti Mzuri N10 | Bimtumwa – 1 |
| 15. | Dimani Pangoni | Ndagoni |
| 16. | Bumbwisudi NB5 | Ziwani |
| 17. | Bumbwisudi NB8 | Gombani – 4 |
| 18. | Kiashange Mzungu | Mwambe |
| 19. | Bambi Pongwe | Mkanyageni |
| 20. | Kipandoni | Mjimbini |
| 21. | Migombani Jeshini | Kironjo D |
| 22. | Dole Mzungu Punda | Kiuyu manda |
| 23. | Tazari | |
| 24. | Kijito Upele | |
| 25. | Mjonga kisima kipya | |
| 26. | Chumbuni | |
| 27. | Masingini | |
| 28. | Kajengwa | |
| 29. | Kiembesamaki kwa Bakathir | |
| 30. | Bumbwini Kidanzini | |
| 31. | Mfenesini | |
| 32. | Bumbwisudi NB5 | |
| 33. | Bumbwisudi NB7 | |
| 34. | Bumbwisudi NB8 | |
| 35. | Bumbwini Uwandani | |
| 36. | Kiashange JP5 – 2 | |

**Kiambatisho nambari 6: Maeneo yaliyofanyiwa Utanuzi na Ukarabati wa Mtandao wa maji**

| Nam | UNGUJA | PEMBA |
|---|---|---|
| 1. | Mpendae | Ukutini |
| 2. | Magomeni | Micheweni |
| 3. | Jang'ombe | Pondeani |
| 4. | Nyaraka | Kangagani |
| 5. | Mtendeni | Mapongwi |
| 6. | Ubago | Mzambarauni |
| 7. | Michamvi | Takao |
| 8. | Welezo | Makongeni |
| 9. | Mwera Hawai | |
| 10. | Zanzibar Park Welezo | |
| 11. | Nyamanzi | |
| 12. | Kombeni hadi Kisakasaka | |
| 13. | Fumba | |
| 14. | Matemwe | |
| 15. | Gulioni | |
| 16. | Bububu | |
| 17. | Mfenesini | |
| 18. | Meli Nne | |
| 19. | Kwerekwe | |
| 20. | Nyarugusu | |
| 21. | Kilimani | |
| 22. | Bumbwini Kidanzini | |
| 23. | Kandwi | |
| 24. | Shakani | |
| 25. | Dimani | |
| 26. | Mwera Pongwe | |
| 27 | Banda Maji | |
| 28. | Munduli | |
| 29. | Mtopepo | |
| 30. | Miembe Saba | |
| 31. | Kipandoni - Kibumbwi | |
| 32. | Amani - Mabata | |
| 33. | Chwaka | |

**Kiambatisho nambari 7: Orodha ya wawekezaji walioonesha nia ya kuekeza katika miradi mbali mbali Zanzibar**

| Nam | JINA LA MWEKEZAJI | ENEO LA UWEKEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | MPS (NORWAY) | Kuwekeza katika uzalishaji wa umeme kutumia nishati ya gesi |
| 3 | ESR | Kuwekeza katika uzalishaji wa umeme wa jua |
| 4 | IDEAL GAS | Kutoa huduma za ushauri elekezi na kuwekeza katika sekta ya nishati mbadala Zanzibar |
| 5 | KUNSONS CONSULTING | Kutoa huduma za ushauri elekezi wa miradi ya nishati Zanzibar |
| 6 | UNIHA | Kuwekeza katika matibabu ya rasilimali maji na uzalishaji wa maji safi kutumia maji chumvi. |
| 7 | TANLUX Co. Investment | Kuwekeza katika uzalishaji wa umeme wa jua na kuwekeza katika kiwanda cha kuzalisha Solar panel |
| 8 | IIAN TECH | Kuwekeza katika sekta ya nishati mbadala |
| 9 | TBEA | Kuwekeza katika sekta ya nishati mbadala |
| 11 | PERNTELS Co. Limited | Kuwekeza katika kusawazisha umeme mdogo na kupeleka umeme vijijini |
| 12 | ICON PBV | Kuwekeza katika uzalishaji wa umeme wa jua |

**Kiambatisho nambari 8: Maeneo yaliyofanyiwa masawazisho ya umeme mdogo**

| ENEO | | |
|---|---|---|
| **Nam.** | **UNGUJA** | **PEMBA** |
| 1 | Mwera mtofaani | Wawi msikiti kibegi |
| 2 | Polisi Ziwani | Kizimbani |
| 3 | Bububu kihinani | Fidel Castro |
| 4 | Mwanyanya kwa Goa | Jadida |
| 5 | Fuoni michenzani | Vikunguni |
| 6 | Kihinani ngalawa | Gando magogoni |
| 7 | Kihinani kikaangoni | Jonza mtambile |
| 8 | Dole wazazi | Pembeni miburani |
| 9 | Mwera batini | Gombani ya kati |
| 10 | K/Samaki mji mpya | Shengejuu |
| 11 | Chuini mkoroshoni | Kipapo |
| 12 | Fuoni chunga | Bubujiko Wete |
| 13 | Nungwi mnarani | |
| 14 | Amani magogoni | |
| 15 | Chukwani buyu | |
| 16 | Chukwani pwani | |
| 17 | Masingini bondeni | |
| 18 | Mbuzini kanisani | |
| 19 | Mtoni basra | |
| 20 | Mtoni matopeni | |
| 21 | Nyamanzi batini | |
| 22 | Fuoni mambosasa | |
| 23 | Shakani kwa mremi | |
| 24 | Masingini magharibi | |
| 25 | Mahonda mto mchanga | |
| 26 | Tunguu kwa pazi | |
| 27 | Masingini kwa Abiola | |
| 28 | Dunga zuze | |
| 29 | Mahonda kituo cha Afya | |
| 30 | Bwejuu tangini | |
| 31 | Bumbwini dundua | |
| 32 | Nyamanzi | |

| ENEO | | |
|---|---|---|
| **Nam.** | **UNGUJA** | **PEMBA** |
| 33 | Fuoni ngome | |
| 34 | Mbuzini kitundu | |
| 35 | Kianga flower | |
| 36 | Bumbwini mbirimbini | |
| 37 | Bwejuu mzungu simba | |
| 38 | Ndunduke | |
| 39 | Kisauni kigorofani | |
| 40 | Kiwengwa polisi | |
| 41 | P/Mchangani | |
| 42 | Kisakasaka | |
| 43 | Kianga chemani | |
| 44 | Meli 4 masumbani | |

**Kiambatisho nambari 9: Maeneo mapya yaliyofikishiwa huduma ya umeme Zanzibar**

| ENEO | | |
|---|---|---|
| **Nam.** | **UNGUJA** | **PEMBA** |
| 1 | Matemwe | Mvimbe Pandani |
| 2 | Kisakasaka | Waani na Shangini |
| 3 | Bwejuu Dongwe | Maambani |
| 4 | Fuoni Birikani | Makaani Kojani |
| 5 | Kiboje Mkwajuni | Kigongoni na Mpambani Chimba |
| 6 | M/Pwani Slave Chamber | Bandamaji Mchangamdogo |
| 7 | Mwera Koani | Wingwi Kongo |
| 8 | Nyamanzi Kusini | Jitenge Shungi na Mwanatojo Mauleni |
| 9 | Kizimkazi Mkunguni | Ndaambani Konde |
| 10 | Kidoti | Bandamaji |
| 11 | Matemwe Kijini | Shumba mjini |
| 12 | Matemwe Kongeni | Mpambani na Kigongoni |
| 13 | Pete Chimbechimbe | Mambosasa |
| 14 | Mfenesini Vuga | Wawi mtega |
| 15 | Ndijani Muembepunda | Tangoni limbani |
| 16 | Uzi Kishagani | Temi |
| 17 | Mtule Mianzikumi | Mnazi mmoja na Mtofini |
| 18 | Mtule Kipanyoni | Raha leo na Mliani |
| 19 | Uzi Uwandani | Kilima hodi jitenge |
| 20 | Kibumbwi | Tumbe mwisho wakijiji |
| 21 | Kipandoni msikitini | |
| 22 | Shakani askari jamii | |
| 23 | Bumbwini Uwandani | |
| 24 | Muyuni kubwa | |
| 25 | Bambi mikarafuuni | |
| 26 | Machui uwandani | |
| 27 | Donge wadi ya kipange | |
| 28 | Mndo madafu | |
| 29 | Binguni | |

**Kiambatisho nambari 10: Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

| | MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA | | | KAZI ZA MAENDELEO | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| PROGRAMU KUU/ PROGRAMU NDOGO | MSHAHARA | RUZUKU YA MSHAHARA | UENDESHAJI WA OFISI (OC) | MAKISIO YA SMZ | MHISANI | RUZUKU | JUMLA |
| **USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI** | | **3,608,200,000** | | **8,652,284,000** | **72,416,837,232** | **-** | **84,677,321,232** |
| Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji | | 3,608,200,000 | | 8,652,284,000 | 72,416,837,232 | | **84,677,321,232** |
| **USIMAMIZI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MADINI** | **430,091,000** | | **230,400,000** | **5,500,000,000** | **5,745,000,000** | **458,516,000** | **12,364,007,000** |
| Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati | 430,091,000 | | 178,343,000 | 5,500,000,000 | 5,745,000,000 | 458,516,000 | **12,311,950,000** |
| Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Madini | | | 52,057,000 | | | | **52,057,000** |
| **UENDESHAJI NA URATIBU WA MIPANGO YA WMNM** | **806,709,000** | | **787,200,000** | | | | **1,593,909,000** |

| MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA | | | | KAZI ZA MAENDELEO | | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| PROGRAMU KUU/ PROGRAMU NDOGO | MSHAHARA | RUZUKU YA MSHAHARA | UENDESHAJI WA OFISI (OC) | MAKISIO YA SMZ | MHISANI | RUZUKU | |
| Utawala na Uendeshaji wa WMNM | 336,264,000 | | 381,800,000 | | | | **718,064,000** |
| Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za WMNM | 93,951,000 | | 215,880,000 | | | | **309,831,000** |
| Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za WMNM - Pemba | 376,494,000 | | 189,520,000 | | | | **566,014,000** |
| **JUMLA KUU** | **1,236,800,000** | **3,608,200,000** | **1,017,600,000** | **14,152,284,000** | **78,161,837,232** | **458,516,000** | **98,635,237,232** |


52
WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI